






# Adhabu

## Punition

-  Adelheid Marie Bwire
-  Melany Pietersen
-  Monica Shank Lauwo, Lauwo George
-  Kiswahili / French
-  Level 2

(imageless edition)






Siku moja, mama alileta matunda mengi.

...


Un jour, Maman a ramassé beaucoup de fruits.



“Tutakula matunda lini?” tunauliza.  
“Tutakula matunda leo jioni,”  
mama anasema.

...


Nous lui demandons : « Pouvons-nous manger des fruits ? » Maman répond : « Nous les mangerons ce soir. »



Kaka yangu Rahim ni mlafi.  
Anaonja onja matunda yote.  
Anakula matunda mengi.

...

Mon frère Rahim est glouton. Il  
goûte tous les fruits. Il en mange  
beaucoup.



“Angalia Rahim alichokifanya!”  
mdogo wangu analalamika kwa  
sauti. “Rahim ni mtundu na  
mchoyo,” ninasema.

...


« Regarde ce qu’a fait Rahim ! »,  
crie mon petit frère. Et moi, je dis :  
« Rahim est méchant et égoïste. »



Mama amekasirishwa na Rahim.

...


Maman est fâchée contre Rahim.



Sisi pia tumekasirishwa na Rahim.  
Lakini Rahim haombi msamaha.

...

Nous aussi, nous sommes fâchés  
contre Rahim. Mais Rahim ne  
regrette rien.




“Hutamwadhibu Rahim?” mdogo wangu anauliza.

...

« Tu ne vas pas punir Rahim ? », demande Petit Frère.






“Rahim, muda si mrefu utajuta,”  
mama anaonya.

...


« Rahim », prévient maman, « tu le  
regretteras bientôt. »



Rahim anaanza kuhisi kuumwa.

...


Rahim ne se sent pas bien.



“Tumbo langu linauma sana,”  
Rahim ananong’ona.

...


Il gémit : « J’ai mal au ventre ! »



Mama alijua hili litatokea. Matunda  
yanamwadhibu Rahim!

...

Maman savait que cela arriverait.  
Ce sont les fruits qui punissent  
Rahim !



Baadaye, Rahim anatuomba msamaha. “Kamwe sitakuwa mlafi tena,” anaahidi. Na sote tunamwamini.

...

Plus tard, Rahim vient s’excuser et promet : « Je ne serai plus jamais aussi glouton. » Et nous, nous le croyons.



# Storybooks Canada

[storybookscanada.ca](http://storybookscanada.ca)

**Adhabu**

**Punition**

Written by: Adelheid Marie Bwire

Illustrated by: Melany Pietersen

Translated by: (sw) Monica Shank Lauwo, Lauwo George, (fr) Suzanne Alban, Translators without Borders

This story originates from the African Storybook ([africanstorybook.org](http://africanstorybook.org)) and is brought to you by [Storybooks Canada](http://Storybooks Canada) in an effort to provide children's stories in Canada's many languages.



This work is licensed under a Creative Commons  
[Attribution 3.0 International License](https://creativecommons.org/licenses/by/3.0/).